

TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



TAARIFA KWA UMMA

MAAMUZI YA TUME KUHUSU VYUO VIKUU VILIVYOKUWA VIMESITISHWA KUDAHILI WANAFUNZI WAPYA KUTOKANA NA MAPUNGUFU MBALIMBALI YA UBORA

1.0 Utangulizi

Itakumbukwa kwamba mwaka 2016 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ilifanya ukaguzi maalum wa kuhakiki ubora katika vyuo vyote vya elimu ya juu nchini. Matokeo ya ukaguzi huo yalibainisha kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika baadhi ya vyuo zinazoathiri utoaji wa elimu bora.

Ili kuimarisha ubora wa elimu itolewayo, Tume imeendelea kufanya ukaguzi wa kawaida na wa kushtukiza katika vyuo vikuu kwa mujibu wa sheria na taratibu za vyuo vikuu. Vilevile Tume imeendelea kuvishauri na kuelekeza vyuo vilivyokutwa na mapungufu kufanya marekebisho kwa kuvipatia muda maalumu kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Vyuo ambavyo vimekidhi viwango vya ubora vimepewa idhini kuendelea na utoaji wa mafunzo, vile vilivyoshindwa vimendelea kuzuiwa kudahili wanafunzi wapya na kuendelea kuwa chini ya uangalizi maalum wa Tume.

2.0 Maamuzi ya Tume

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ilifanya vikao viwili katika mwezi wa Juni 2019, kikao cha 89 tarehe 8 Mei, 2019 na kikao maalum cha 91 tarehe 18 Juni, 2019. Katika vikao hivyo Tume ilijadili na kuchambua ripoti zilizowasilishwa na vyuo vilivyokuwa vimesitishwa kudahili wanafunzi wapya. Tume ilijiridhisha kwamba baadhi ya vyuo vimekidhi vigezo vya ubora na baadhi ya vyuo vimeendelea kuwa na changamoto ambazo zinaathiri ubora wa elimu. Hivyo Tume ilifanya maamuzi yafuatayo matatu makubwa, ikiwa ni kufuta usajili, kutoa idhini ya udahili, na kuendelea na uangalizi kwa baadhi ya vyuo.

2.1. Imefuta Hati ya Usajili (Certificate of Full Registration) ya Chuo Kikuu Cha Eckernforde Tanga

Tume imefuta Hati ya Usajili wa Chuo Kikuu cha Eckernforde Tanga kuanzia tarehe 18 Juni, 2019. Hivyo kutokana na kufutwa kwa Hati hiyo ya Usajili, Chuo Kikuu cha Eckernforde Tanga kimeondolewa katika daftari la vyuo vikuu nchini.

2.2. Imeruhusu Vyuo Vikuu sita (6) kuendelea na utoaji wa mafunzo na kudahili wanafunzi wapya kwenye baadhi ya programu za masomo kuanzia mwaka wa masomo 2019/2020

Tume imejiridhisha kwamba vyuo vifuatavyo vimerekebisha mapungufu ya ubora yaliyokuwa yamebainishwa hapo awali na kukidhi vigezo vya ubora kwa mujibu wa miongozo iliyopo. Hivyo Tume imeruhusu Vyuo sita (6) kuanza kudahili wanafunzi wapya kwa baadhi ya programu za masomo kuanzia mwaka wa masomo 2019/2020.

1. Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mihayo Tabora (AMUCTA) – programu tatu (3)
 - a) Bachelor of Arts with Education;
 - b) Bachelor of Education (Special Needs); na
 - c) Bachelor of Business Administration.
2. Chuo Kikuu cha Umoja wa Afrika nchini Tanzania (UAUT) – programu mbili (2)
 - a) Bachelor of Business Administration; na
 - b) Bachelor of Science in Computer Engineering and Information Technology.
3. Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (TEKU) – programu mbili (2)
 - a) Bachelor of Education Languages; na
 - b) Bachelor of Divinity.
4. Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano Moshi (SMMUCo) – programu moja (1)
 - Bachelor of Accounting and Finance
5. Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala nchini Tanzania (KIUT) – programu tano (5)
 - a) Bachelor of Social Work and Social Administration;
 - b) Bachelor of Laws;
 - c) Bachelor of Business Administration (Accounting; Commerce; Finance and Banking);
 - d) Bachelor of Computer Science; na
 - e) Bachelor of Public Administration.

6. Chuo Kikuu Kishiriki cha Marian (MARUCo) – programu mbili (2)
 - a) Bachelor of Science in Mathematics and Statistics; na
 - b) Bachelor of Education in Science (Mathematics and Physics).

Ifahamike kwamba baadhi ya programu za masomo katika vyuo hivi ambazo hazijaorodheshwa katika taarifa hii zimeendelea kuzuiwa kudahili wanafunzi wapya kwakua bado hazijakidhi vigezo vyta ubora kwa mujibu wa miongozo iliyopo.

2.3. Vyuo Vikuu ambavyo bado vimezuiwa udahili wa wanafunzi wapya na kupewa muda kukamilisha utekelezaji wa maelekezo ya Tume

Tume imeendelea kuzuia udahili wa wanafunzi wapya kwa ngazi zote za masomo kwa programu zote kwenye Vyuo Vikuu vitatu (3). Vyuo hivi vimepewa muda wa miezi sita kukamilisha utekelezaji wa maelekezo ya Tume:

- a) Chuo Kikuu cha Bagamoyo (UoB);
- b) Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU); na
- c) Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mt. Fransisko (SFUCHAS).

Vyuo hivi vitaendelea kuwa chini ya uangalizi maalumu wa Tume, haviruhusiwi kudahili wanafunzi wapya kwa ngazi zote za masomo (kuanzia astashahada, stashahada, shahada, shahada ya uzamili, hadi Shahada ya Uzamivu) kwenye programu zote za masomo.

3.0 Hitimisho

Bado kuna Vyuo vilivyokuwa vimesitishwa udahili wa wanafunzi wapya ambavyo havikutajwa katika taarifa hii. Tume inaendelea na uhakiki na uchambuzi wa taarifa zao za utekelezaji na taarifa kuhusu hatma ya vyuo hivyo itatolewa hivi punde.

Imetolewa na



KATIBU MTENDAJI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)

15 Julai 2019